TANGAZO LA SERIKALI Na. 492 la tarehe. 14/6/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),
(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO YA ULINZI WA UMMA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KONDOA YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ulinzi wa Umma ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa;

"Kamanda" maana yake ni kiongozi wa kikundi cha ulinzi katika kitongoji au kijiji;

"Kamanda Msaidizi" maana yake ni kiongozi msaidizi wa kikundi cha ulinzi katika kitongoji au kijiji;

"mkazi" maana yake ni mtu yeyote ambaye anaishi ndani ya eneo la Halmashauri.

Wajibu wa kushiriki katika ulinzi

4. Kila mkazi wa Halmashauri mwenye umri wa zaidi ya miaka kumi na nane atawajibika kushiriki katika shughuli za ulinzi wa umma kama itakavyoratibiwa na uongozi wa kijiji, kata, Halmashauri au Jeshi la Polisi kwa kadri itakavyofaa na atawajibika kufanya mambo yafuatayo:

(a) atashiriki ulinzi yeye mwenyewe kwa mujibu wa utaratibu utakaokuwa umepangwa na uongozi wa kitongoji au kijiji chini ya usimamizi wa Kamati ya Maendeleo ya Kata;
(b) kaya yake itachangia kiasi cha fedha kitachoidhinishwa na Halmashauri, Halmashauri ya kijiji au uongozi wa kitongoji kutegemeana na hali halisi kwa ajili ya kugharamia shughuli za ulinzi.

Kuanzisha kikundi cha ulinzi

5. Kikundi cha ulinzi kitaanzishwa katika kila kijiji au kitongoji ndani ya Halmashauri kwa lengo la kuimarisha ulinzi kwa ushirikiano na Jeshi la Polisi.

Kiongozi wa kikundi

6. -(1) Kila kikundi cha ulinzi kitakuwa na kiongozi atakayetambuliwa kama Kamanda wa kikundi ambaye atateuliwa kutoka miongoni mwa watu wanaounda kikundi cha ulinzi cha kijiji au kitongoji.

(2) Kamanda wa kikundi atakuwa na msaidizi wake atakeyejulikana kama Kamanda Msaidizi wa kikundi ambaye atateuliwa kutoka miongoni mwa watu wanaounda kikundi cha ulinzi cha kijiji au kitongoji.

Wajibu wa kamanda kuandaa orodha ya wakazi

7. Kila kamanda wa kikundi atatakiwa kuwa na orodha ya wakazi wote wanaostahili kushiriki katika shughuli ya ulinzi ndani ya kijiji au kitongoji na orodha hiyo itahifadhiwa katika daftari maalumu na kutunzwa katika ofisi za kata au kijiji.

Wajibu wa Kamanda kuwasilisha taarifa

8. Kila Kamanda wa kikundi cha ulinzi atawajibika kusimamia kikundi kitakachokuwa zamu kwa siku husika na kuwasilisha orodha ya walinzi waliopo zamu katika ofisi ya kata au kijiji ambapo kikundi cha ulinzi kipo.

Makosa

9. Mtu anatenda kosa iwapo-
(a) hatashiriki katika shughuli za ulinzi;
(b) anakataa au kukwepa kushiriki katika ulinzi;
(c) anamshawishi mtu au kikundi cha watu wasishiriki katika ulinzi; au
(d) anamzuia Kamanda au msaidizi wake

kutekeleza majukumu yake.

Adhabu

10. Mtu atakayetiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi elfu hamsini na kisichozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote.

Kufifilisha kosa

11. Mkurugenzi anaweza kumtoza faini mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii, kiasi cha shilingi elfu hamsini ikiwa mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 11)*

FOMU YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi.........…………………….......................................…………. Nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya …………………………………..… ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa kwamba mnamo tarehe…………ya Mwezi…......... Mwaka ……………. nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya ………. ya Sheria Ndogo ya Ulinzi wa Umma ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ya Mwaka 2024.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, Niko tayari kulipa kiasi cha Shilingi……...........……… kwa ajili ya kufifilisha kosa nililotenda chini ya Sheria Ndogo ya Ulinzi wa Umma ya Mwaka 2024.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.

Leo tarehe……...................…..ya Mwezi……………………Mwaka…………………..
Jina………………………...............……..…………….Saini……………………….

MBELE YA:
Jina……………………………………………….…..
Wadhifa……………………..……………………….…..
Saini…………………………………………………
Tarehe……………………………………………….

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa imegongwa kwenye Sheria Ndogo hii kufuatia Azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa uliofanyika tarehe 28/4/2022 na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya:-

SHABAN KAPALA MILLAO,
*Mkurugenzi Mtendaji,*
*Halmashauri ya wilaya,*
*Kondoa*

ABDALLAH SALUM MAGUO,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Kondoa*

**NAKUBALI**,

L.S

Dodoma,
25 Machi, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB.),
*Waziri wa Nchi -OR-Tamisemi*